



FOMU YA MAOMBI KITUO ATAMIZI CHA SUA-AIC, MOROGORO

Kabla ya kujaza fomu, soma maelezo kuhusu sifa za muombaji, masharti ya kuomba na jinsi ya kujaza fomu, na kuwasilisha fomu iliyopo chini

- Sifa za Kijana zinazotakiwa: Ueledi wa ujasiriamali, maarifa, mwenye uzoefu kwenye kilimo na kilimobiashara, awe na tabia njema, utii, nidhamu, mchapa kazi, fikra chanya, mwaminifu na anayependa kuona matokeo chanya. Vijana wa kike wanapewa kipaumbele.
- Fomu ya maombi inapatikana kwenye tovuti za AIC (www.aic.co.tz) na PASS (www.pass.or.tz); ofisi ya SUA/SAEBS (Morogoro) na ofisi zote za PASS (Dar, Arusha, Morogoro, Mbeya, Kigoma, Mtwara, Mwanza, na Kongwa); na kwenye Maonesho ya Nane Nane mikoa ya Simiyu, Morogoro, Mbeya, Arusha (mabanda ya PASS) na Dodoma (banda la TALIRI).
- Ada ya fomu ni shs 10,000/- Ada hiyo ilipwe kwenye akaunti ya PASS, benki ya CRDB.
 - Namba ya Akaunti: 01J1076972802
 - Jina la Akaunti: Private Agricultural Sector Support
 - Tawi: Morogoro
 - Taja jina lako ikifuatiwa na '**Kituo Atamizi SUA-AIC**' kwenye kumbukumbu ya malipo (Bank slip); kwa mfano: 'Fatuma James – Kituo Atamizi SUA-AIC'
 - Ada hiyo haitarejeshwa hata kama mwombaji hatachaguliwa.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 12/08/2019.
- Mchakato wa maombi utajumuisha: Kujaza fomu, kulipa ada, na kuwasilisha fomu pamoja na kumbukumbu ya malipo kwa PASS AIC.
- Baada ya PASS AIC kupokea fomu; watachaguliwa vijana 200, watakaotakiwa kufika Morogoro mjini kwa muda wa siku 7 kushiriki kwenye mchujo wa awamu ya pili. Hatua ya mwisho ya mchakato baada ya mchujo wa pili ni kuchaguliwa kwa vijana 70 watakaoshiriki kwenye Kituo Atamizi kwa kipindi cha miezi 12 kuanzia mwezi Oktoba 2019.
- Kijana atakayeshiriki kwenye mchakato wa mchujo wa awamu ya pili utakaofanyika Morogoro mjini, atatakiwa kujikimu kwa gharama zake binafsi zikiwemo nauli, malazi na chakula.
- Unaweza kutuma fomu pamoja na stakabadhi ya malipo kwa baruapepe kwenda maombi@aic.co.tz, au kwa kupeleka kwenye ofisi za PASS iliyopo karibu nawe.



FOMU YA MAOMBI – KITUO ATAMIZI CHA SUA-AIC MOROGORO

1	Jina	
2	Barua pepe	
3	Simu	
4	Anwani	
5	Kijiji / Kata / Mji / Mkoa	
6	Jinsia (Kiume / Kike)	
7	Umri	
8	Hadhi ya Ndoa (chagua moja)	Sijaoa / Nimeoa-olewa / Nimeachika / Mjane / mengineyo
9	Elimu (chagua moja)	Darasa la 7 / Kidato cha 4 / Kidato cha 6 / Chuo / Sina elimu
10	Uzoefu wako juu ya kilimo (Taja / Toa maelezo)	
11	Uzoefu wako juu ya Kilimobiashara (Taja / Toa maelezo)	
12	Shughuli kuu ya kiuchumi unayofanya/jihusisha nayo (chagua unayofanya; toa maelezo ya kina)	Uzalishaji wa mazao / ufugaji / usindikaji / biashara / sina shughuli
13	Kwa nini unataka kujiunga na Vituo Atamizi vya PASS AIC? (Toa maelezo)	